
# NGURUMO ya MWANDISHI




Toleo la III-DESEMBA-MMXXI

**Mwaka 2022 uwe wa mapinduzi ya kalamu**

## Dawati la Mhariri: Mwaka 2022 uwe wa mapinduzi ya kalamu

0766-974 865

Awali ya yote, napenda kuwatakia heri sana ya mwaka mpya wa 2022.

Sote tumefurahi kuuanza mwaka huu mpya wa 2022 kwa moyo wote. Tumshukuru Mungu kwa kuwa tumefika salama ukizingatia dunia ipo kwenye tashwishwi inayoletwa na ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Corona.

Sote tumekuwa mashuhuda, ama tumeondokewa na ndugu, jirani au hata rafiki. Hivyo basi bado twapaswa kuchukua tahadhari ya kila hali hasa sasa ambapo wimbi la nne 'Omicron' limeivamia dunia. Tumwambie Mungu asante kwa kuwa hai hata sasa.

Tukiachana na hilo, mwaka wa 2021 naweza kusema umekuwa wa mafanikio katika tasnia hii ya uandishi. Tumeshuhudia waandishi wakizindua vitabu na kuijengea heshima tasnia hii. Tunawashukuru wote waliofanikiwa katika hilo. Lakini pia tumeshuhudia kongamano kubwa la waandishi wa Afrika ambalo limefanyika hapa Tanzania. Licha ya hilo waandishi na wadau wa fasihi hapa nchini wamefanya mengi katika kutangaza na kuikuza tasnia hii.

Tusiishie hapo; mwaka huu mpya wa 2022 uwe wa mapinduzi ya kalamu. Waandishi tuchape vitabu kwa wingi ili kukata kiu ya wasomaji.

Tusiseme wasomaji hakuna, bali tuongeze nguvu kwenye uchapaji wa vitabu bora na si bora vitabu. Kama tukifanya hili kwa malengo yakinifu yenye tija, basi kalamu itaboresha maisha ya waandishi.

Nikutakieni mwaka mpya mwema na wenye mafanikio kedekede.

## Hanifa Kafashe, ageukia malezi ya watoto wa kiume



**Hanifa Kafashe**

Ukiingia katika mtandao wa kijamii wa *Facebook*, huwezi kuperuzi kuta zaidi ya tatu kabla hujakutana na huyu anayejiita Malkia wa Kiha kwa rakabu yake na jina halisi ni Hanifa Kafashe. Yeye ndiye mtunzi na mwandishi wa kitabu kilichobeba jina Tunu Sita za Malezi.

Ngurumo ya Mwandishi baada ya kunusanusa na kupata fununu ya kuwa kuna chapisho mujarab linapikwa na mwanamama huyu mwenye mvuto wa kipekee, halikusita kumuuliza. Naye akakiri kuwa mwaka 2022 mambo yatakuwa moto.

Yeye mwenyewe kwa kinywa chake anaeleza. Nanukuu.

"Kumekuwa na mstari mwembamba unaotofautisha malezi ya watoto wetu wa kike na kiume. Na isivyo bahati, pengine kwa ufinyu wa mstari huo, wazazi wengi hawauoni, na kama wanauona basi wanaupuuzia na kuhisi kwamba hautakuwa na madhara yoyote huko mbele ya safari.

Kwa kuzingatia hilo, nimeamua kuandika kitabu kinachomfundisha mtoto wa kiume kujitambua kama mwanaume, kujua umuhimu wa nafasi ya kuzaliwa kwake katika familia na kutambua umuhimu wa uongozi kuanzia hapo nyumbani. Zaidi nataka nimjuze kutambua jinsi ya kuutunza na kuulinda uanaume wake.

Kitabu hiki kitamfanya mtoto wa kiume aheshimu thamani ya mwanamke yeyote kuanzia nyumbani, shuleni mpaka mtaani na mambo mengine kadha wa




kadha ambayo kisaikolojia yatamfanya kuwa bora hata katika nidhamu ya fedha kuanzia utafutaji mpaka matumizi.

Licha ya yote, sijaacha kumhasa mtoto huyu wa kiume juu ya kujua afya yake katika mgawanyiko wa kimazingira na kihisia ambavyo vitamsaidia katika kuiboresha afya yake ya akili na kumfanya apate ustawi wenye kustahili".

Mwandishi ni miongoni mwa wanawake wachache wanaopambania malezi ya watoto na ustawi wa mambo ya kijinsia. Daima huutumia ukuta wake wa *facebook* kuzungumza ukweli wa mambo yaendayo kinyume na malezi bora ya watoto.

Kelele zake za kila siku ni kumtaka mwanaume au mwanamke ajitambue nafasi yake katika jamii na si kudai haki zisizomstahili.

# Wilbard Makene aja na Kifurushi Ikulu

**Na: Richard Mwambe**

Fasihi inazidi kupaa. Unaweza kujiuliza kwa nini nasema hivyo! Hautakosea.

Mwezi uliopita tulishuhudia uzinduzi wa kitabu cha Miss Tz pale Hoteli ya Peacock, Dar es salaam. Shughuli kama hii haikuishia hapo. Waandishi wameamua kuipa heshima sanaa yao.

Wilbard Makene, mwandishi wa kitabu cha Sarafu ya Gavana amezindua kitabu kipya kinachokwenda kwa jina Kifurushi Ikulu. Tafrija hiyo iliyofanyika katika hoteli ya Protea Courtyard Oysterbay ilihudhuriwa na wapenzi wa riwaya kutoka pande zote za Tanzania wakiongozwa na mwandishi Yeriko Nyerere.

Kifurushi Ikulu ni riwaya ya pili ya Wilbard kuingia kwenye kitabu baada ya ile Sarafu ya Gavana.

"Uzinduzi huo ulikuwa wa kipekee sana, kwani wasomaji walilipia nakala zao mapema kabla hata ya kufika ukumbini." ameeleza Eliado Tarimo aliyemwakilisha Rais wa UWARIDI. Eliado aliendа mbali zaidi kwa kueleza umuhimu wa waandishi kuwa na dira iliyobebwa na mikakati thabiri katika kuboresha na kuikuza tasnia hii.

Naye Yeriko Nyerere alikielekezea kitabu hicho kuwa, kwa jina lake tu ni taharuki tosha na kitatuvuta kujua nini




kipo ndani yake.

Tukio hilo lilihudhuriwa pia na waandishi mbalimbali akiwamo nguli Richard Mabala na mwandishi mashuhuri wa hadithi za watoto Bi. Nahida Ismail, mshindi wa tuzo nne za CODE kwa fasihi ya Afrika.

Mwandishi pendwa, Hussein Molito aliyekuwa mmoja wa waliohudhuria kwenye hafla hiyo aliliambia gazeti hili, "Ni maendeleo kwa Tasnia ya uandishi. Ni tukio kubwa ambalo nimepata bahati ya kuhudhuria pia.

Moja ya vitu nilivyojifunza kwenye uzinduzi wa kitabu cha Kifurushi Ikulu; kwanza ni thamani ya kitu ambacho mtu umeamua kukifanya ya inavyopanda kwa kadri ulivyowekeza. Pili inakupa mawanda mapana ya kukutana na wadau wa tasnia husika.

Nimegundua hata waandishi wanaweza kufanya makubwa na vyombo vya habari vikapata habari".

Zaidi ya hilo mwandihi Molito anakazia kuwa tukio la uzinduzi na utiajisaini kitabu cha Kifurushi Ikulu ulikuwa bora sana kwa jinsi mtiririko wa ratiba na matukio ulivyopangwa.

Wilibard Makene anatujuza kuwa kitabu hiki sasa kinapatikana kwenye maduka mbalimbali ya vitabu nchini na zaidi kinapatikana kwenye mtandao wa Lantern e-books unaopatikana ndani ya tovuti www.lantern.co.tz

*Sisi tunaandika na wewe usome.*

**0766 974 865**

Penda kusoma vitabu

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI


Faida za kusoma vitabu:

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Uboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Ukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Uboresha Mtazamo na Umakini



# Mwandishi Model Teddy atuahidi mazuri 2022

**Anaandika Teddy Andrew**



**"Model Teddy"**

**2020 _2021 hazikuwa nzuri kwa upande wangu hasahasa eneo hili laundishi. Niliamua kubaki kimya kwanza toka June 2020 hadi *December* hii ili kuwa sawa kwanza.**

Haikuwa miaka mizuri kwangu ndani ya uandishi kwani mwili, akili na moyo havikuwa sawa hata kidogo.

Nilikuwa nikijaribu mara kwa mara kuandika lakini nilishindwa na mara nyingi niliharibu kazi, nilikuwa naandika na kujaribu kusoma mwenyewe naona mbaya, kama mie mwandishi naona mbaya vipi kwa upande wako msomaji.

Wengi wamenifuata *inbox,* wamepiga simu kuulizia vipi mbona kimya niliwajibu kiaina tu nitarejea ama nalea au nipo.
Kukaa kimya pasina kupost kulipelekea hata page kufungwa la kushangaza haikuniuma niliona kawaida tu.

Sikuipenda ile hali ya kushindwa kuchapa, nilijabu na kujaribu lakini nilishindwa, kuna muda militoa chozi nilitamani nipate msaada lakini sikupata kiukweli niliumia mno na mno. Na upata wapi na nani wa kuyaficha haya yangu maana kuna rafiki wa shida na raha halafu mwisho wa siku inakuwa shida tena

Nikawa mtu wa hasira za haraka pindi niliposhindwa kutelekeza jambo lolote, mkimya kama fala mpya, nilichoamua ni kufungia PC ndani na kuacha kila kitu nikajikita zaidi kusoma kazi za wenzangu kimya kimya.

Nikajaribu kujipa furaha japo nayo nilikuwa ngumu, April ndipo nilipogundua ni kipi kilipelekea mie kuwa vile MSONGO WA MAWAZO.


Umenichukua kwa kipindi kirefu toka ujauzito ambao nao ulikuwa wa misukosuko chungu nzima, yote tisa now niko poa nimepona kwa msaada wa mtu mmoja hivi ambaye amenisha mkono toka hiyo April hadi hii December.

Naimani 2022 kwa uweza wake Mungu nitarejea rasmi huku, nisamehewe tu kwa udanganyifu nilioufanya wa kusema narejea muda wowote lakini nilishindwa kufanya chochote. Mengi yametokea kwangu, mengi yameniliza, mengi yamenirudisha nyuma, lakini yote kwa yote ni njia ya kujifunza, kukomaa zaidi

Amani ya moyo ni kitu muhimu mno.

*Ciao!*

## Je; kusoma ni muhimu katika maisha yetu? - 3



**Na: Mwandishi wetu**

Katika matoleo yetu mawili yaliyopita, tuliangalia kiujumla umuhimu wa kusoma. Lakini leo tutasonga mbele na kutazama faida za usomaji wa vitabu na makala anuai. Wapo ambao hawaamini kuwa kuna faida kubwa katika usomaji wa vitabu. Wenyewe wasomaji wana ushuhuda.

Kusoma vitabu kuna faida nyingi sana, lakini hapa tutazungumzia faida kumi kadiri ya watafiti mbalimbali

**1—Msisimko wa akili**

Watafiti wanatuambia kuwa, kubaki na msisimko wa akili kunaweza kupunguza au kuepusha ugonjwa wa kusahau (Alzheimer's & Dementia) kwa kuwa unauweka ubongo wako katika umakini na unafanya usipoteze nguvu.

Kama ilivyo kwa msuli wowote wa mwili, ubongo unahitaji mazoezi ili uwe na nguvu na afya,. Hivyo kusoma ni moja ya mazoezi ya kuusisimua ubongo. Pia aina nyingine za mazoezi ya kuusisimua ubongo ni kama vile kucheza drafti, bao, karata nk. Hivyo soma vitabu sana uujenge ubongo wako na kuusisimua.

**2– Upunguza msongo wa mawazo**

Haijalishi una msongo wa mawazo kiasi gani huko kazini, kwenye mahusiano yako binafsi au katika mambo yako yanayokukabili kila siku. Haya yote yatafutiliwa mbali kama ukizama kwenye kitabu cha hadithi fulani ya kuvutia. Kitabu cha hadithi kilichoandikwa vizuri kitakuhamisha na kukupeleka kwenye uhalisia mwingine wakati ukizama kwenye makala tamu itakuweka katika wakati uliopo, vitaondoa hali uliyonayo na kukuacha urelax.


***Itaendelea toleo lijalo...***

## MSETO WA MAJI MANDIGA, MANDIGA KOMIKI MPAKA MANDIGA'S WELL

**Na: Richard Mwambe**

Uandishi wa vitabu nchini Tanzania unazidi kukua tofauti na miaka kumi iliyopita. Kukua kwake hakumaanishi tu kuongezeka kwa idadi ya waandishi, bali waandishi wenyewe kufikiria nje ya boksi kwa kuzipeleka kazi zao nje ya mipaka ya Tanzania na kwa mtindo tofauti.


Hilo limejidhihirisha kwa mwandishi Mohammed Hammie




Rajab kupitia kitabu chake cha Maji Mandiga, ambacho huenda ndio kimesomwa zaidi kwa mwaka wa 2021.
Wakati wa mahojiano na jarida hili Mohammed anasema kuwa, simulizi ya kwenye kitabu cha Maji Mandiga angependa kuiona kwenye mitindo mbalimbali ya usimuliaji ili iwafikie hata wale wasiopenda kusoma vitabu.

"Tunakuwa na hadithi nzuri, lakini mara nyingi huishia kwenye mfumo wa maandishi tu. Si jambo baya, lakini tunawanyima uhondo wale wasiopenda kusoma. Ningependa kuiona simulizi ya Maji Mandiga inaenda kwenye mitindo mingine kama vile mchezo wa redio na hata filamu" amesema Mohammed.
Hivi karibuni kitabu cha Maji Mandiga kilitolewa kwa mtindo wa Komiki. Simulizi kwa picha ambapo iliwafanya hata wale wasiopenda kusoma vitabu iwafikie.

Jarida hilo ambalo lilipata ufadhili kutoka shirika la Simavi la nchini Uholanzi lilikuwa na lengo la kuwafikia zaidi watoto ambao kimsingi hupendelea kujifunza ama kusoma kwa kutazama zaidi picha. Takribani nakala 1,000 zilichapwa na kugaiwa bure mashuleni.
Jarida la Maji Mandiga Komiki limeelezwa kuakisi maisha halisi ya kila siku ya wanawake waishio vijijini nchini Tanzania na maeneo mengine barani Afrika.
Mwandishi ametoa utambuzi wa kipekee katika mtazamo na desturi za wanawake hao na wasichana katika jamii hizo na nafasi zao.
Anayopitia Mandiga yamemuonesha msomaji jamii inayofurahia maendeleo na wakati huo huo changamoto za kufikia






Mohammed Hammie Rajab
Mwandishi wa
MAJI MANDIGA

usawa wa kijinsia na kufurahia matunda ya maendeleo endelevu kwa kila mtu.
Mwandishi ameyanyambua barabara madhila anayoyapitia mwanamke, hatua kwa hatua akionesha namna ambavyo tatizo moja lisipotatuliwa linavyoweza kuzalisha makumi ya matatizo.
Mohammed amesimama kidete kuhakikisha simulizi hii matata ambayo inasadifu vyema yanayoendelea maeneo mengi ya vijijini barani Afrika haishii hapa Tanzania pekee.

"Tayari kitabu kimeshatafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza, kinatarajiwa kuchapwa mwaka huu wa 2022 na nchi za mwanzo kusambazwa ni Tanzania, Nigeria, Ghana na Zimbabwe" amesema Mohammed Hammie wakati wa mahojiano maalumu na jarida hili.
Mohammed ameongeza kwa kusema kuwa, tafsiri ya kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza imefanywa na Mwalimu Richard Mabala, mmoja wa waandishi wanaoheshimika zaidi ndani nje ya Tanzania.

Punde baada ya kitabu cha Maji Mandiga kutafsiriwa kilitumwa nchini Uingereza kwa ajili ya kufanyiwa uhariri kwa ufadhili kutoka shirika la AquaFed ambalo lilimlipa Bi Amanda Harley kwa kazi ya kuhariri.

RIWAYA

# MPIGA MBIO — 03



Richard Mwambe

***Kwa wasomaji wapya...***

***Mlio wa gari analolijua ukasikika kwa mbali. Kwa hesabu zake ilikuwa kama mita mia mbili hivi. Akatega masikio yake kama mbwa aliyehisi mhalifu.***

***Endelea….***

Akasimama taratibu na kulifuata dirisha dogo lililo upande wa baharini, akasogeza pazia kwa chati na kuangalia uelekeo wa barabarani. Naam, alichofikiri ndicho. Subaru jeusi liliipita ile nyumba huku likipiga honi na kuelekea upande wa pili wa msitu ule. Kenneth akasonya na kutoa tusi la moyoni kwa hao waliopita na gari hilo. Hakuna tusi baya kama la moyoni maana mtukanaji hakuchagulii lipi linakufaa na lipi halikufai…

Mara baada ya kurudisha lile pazia mahali pake, Kenneth alivaa koti lake na kujifunika lile kapuchi kichwani kujikinga dhidi ya manyunyu ya mvua. Akatoka nje na kuzunguka nyuma. Hatua baada ya hatua alichapulisha miguu kuelekea mwisho wa ule msitu. Mwendo wa dakika tano hivi, akatokea upande wa pili wa msitu ule. Upande ule kulikuwa na fukwe nzuri na ya kupendeza. Watu wachache waliokuwa wakiogelea waliendelea na shughuli yao. Kenneth aliliona lile Subaru limeegeshwa mbali kidogo.

Upande wa kushoto kwake, kulikuwa na 'kijiwe' ambacho vijana walipenda kuketi kupunga kile walichokiita *'Sea breeze'*. Nyuma yao kulikuwa na kibanda kilichojengwa kwa miti na kuezekwa kwa makuti ya mnazi. Mapambo ya asili na chupa zilizoning'inizwa zilipendesha eneo hilo. Muziki wa Lucky Philip Dube, *'Remember Me'* ulisikika. Kenneth akakunja kona na kuelekea kwenye kile *kijiwe*. Akajichagulia kigogo cha kuketi, akafanya hivyo. "*Peace and Love Bro'*" kijana mmoja akamsalimu kutoka upande wa nyuma yake. "Na kwako pia *man*!" Kenneth akajibu na kunyoosha mkono kwa nyuma kama anataka kupokea kitu. Naam! Sekunde chache tu, chupa ndogo ya konyagi ikatua kiganjani mwake. "*Enjoy your day*!" kijana mwingine akamwambia huku akiketi katika kigogo kilekile. "Mnaniangusha!" Kenneth akamwambia yule kijana aliyeketi naye mara baada ya kupiga funda moja la kinywaji kile, *'Spirit of the Nation'*. "Mazingira yalibana kaka… *mandula* walikuwa makini kinyama, sura za mbu…." kabla hajamaliza kusema, Kenny akamnyoshea mkono kuwa anyamaze. "Unaupiga mwingi jamaa… Hii kazi, kazi haitaki *shobo*, kazi haitaki maneno. Kama unataka na unahitaji pesa piga kazi, mwanaume lazima upigike, ujitoe mhanga kwa ajili yako na familia yako…." akapiga funda jingine, "na demu wako". "Najua lakini mazingira hayakuruhusu, wewe mwenyewe hutuambia kuwa 'shujaa akiona shimo, hurudi nyuma kabla ya kuruka…'" "Sawa!" Kenneth akajibu. Ukimya wa dakika mbili ukampa nafasi ya kumaliza kinywaji chake. "Khaaaaaakh… mmmmm!" akaunguruma kuusindikiza ukalimoto wa kinywaji kile. "Lile tulilopanga miezi mitatu iliyopita tutalifanya mwezi ujao… sasa kila mmoja achukue *chimbo* lake, tutawasiliana kwa njia hiihii, hapahapa," akainuka na kujipukuta mchanga kidogo. Akavuta hatua kuelekea kwenye nyumba yake kule msituni.

********

Siku hii ilikuwa mbaya sana kwa Ikunda. Alikosa hata hamu ya kufanya kazi kwa kutomuona yule mpigambio anayeukuna mtima wake. *Kapatwa na nini leo?* Akajiuliza. Pamoja na hali hiyo aliyokuwa nayo, Ikunda aliendelea na kazi. Majira ya saa nane alasiri , Ikunda alikutana na kitu hasichokitarajia. Kenneth alikuwa ndani ya Benki ya Maendeleo ya Wazaramo, mkononi mwake akiwa na bahasha ya khaki. Kwa haraka Ikunda alijua kuwa mwanaume huyo kaja kuweka akiba ya pesa zake. Hakuwahi kufikiri kama kijana huyo, anamiliki akaunti katika benki hiyo.

Hii kwa Ikunda ilikuwa nafasi, akajaribu kuzichanga karata zake vyema. *Lazima nimtie mkononi!* Alichapukia moyoni. Makusudi, akajipitisha na vifaa vyake vya usafi huku miguu yake akihisi ikigongana. Vazi alilovaa liliuelezea mwili wake. Kenneth alimtazama biti huyo wakati akielekea upande wake, macho yao yakagongana….

***Itaendelea toleo lijalo.***

0766974865

# ADILI NA NDUGUZE

BAADA ya nahodha wa Jahazi kutanabahi kwamba pipa lililohifadhia maji ya kunywa lilikuwa limetoboka na maji yote kuvuja, aliamuru kutua tanga na kutia nanga, ili mabaharia wateremke jabalini kwenda kutafuta maji. Bwana Adili pamoja na ndugu zake wawili; Mwivu na Hasidi, nao walikuwamo jahazini kama wafanyabiashara waliokodisha usafiri huo. Nao walishuka kwenda kutafuta maji.

Katika kuhangaika huku na kule, Adili akiwa juu ya jabali, mara akamwona tandu akikimbizwa na nyoka, hata hakufika mbali, akawa amekamatwa kwa kuumwa kichwani. Kwa milio ya uchungu aliyoitoa tandu, Adili aliingiwa na huruma akaokota jiwe la kiasi cha kama ratili moja hivi, akamponda nyoka kichwani na kufa palepale. Alitoa msaada ule ili kumtetea tandu aliyekuwa taabuni akilalama kukumbwa na nakama. Pengine hivyo ndivyo mwandishi wa kitabui hiki, Shaaban Robert, aliamua kutuasa wanaadamu namna ya kuishi, kwa kujiweka tayari muda wote ili kusaidia pale haki ya yeyote inapopokonywa.

Kinyume na matarajio ya Adili, badala ya tandu kukimbia baada ya kuponea chupuchupu, taratibu alianza kubadilika kutoka tandu na kuwa kiumbe kisichoeleweka. Kutahamaki akawa msichana mzuri aliyesimama mbele ya Adili. Msichana huyo, alimsogelea Adili akampa mkono wa shukrani huku akimwombea dua. Na baada ya hapo, alielekeza kidole chake ardhini, ardhi ikapasuka akapotelea humo. Kitambo kidogo, yule nyoka aliyekufa alianza kuwaka moto na kuteketea kabisa hata akabaki majivu matupu. Na katika hali ya kustaajabisha, mahala pale palipobaki majivu hayo pakageuka chemchem ya maji safi. Kwa muujiza huo, Adili alikiri kwamba msichana yule hakuwa mwanaadamu bali ni Jini. Si Adili tu, bila shaka hata mimi na wewe tungelifikiri namna hiyo. Basi Adili akafanya hima kwenda kuwafahamisha wenziye juu ya ugunduzi wake wa maji. Wote wakafurahi. Wakajumuika pamoja kuchota maji, kisha wakaendelea na safari.

Baada ya safari ndefu ya mchana




na usiku, walipoteza tena mweleKeo hata wasiione bara wala kisiwa. Wakaanza kutaabika. Isivyo bahati, maji yakawaishia tena. Nahodha akaanza kutafuta namna ya uwokovu wao. Na baada ya kuona jabali lingine, tanga liligeuzwa haraka na mara moja wakatua. Hapo tena wakaanza kuhangaika kutafuta maji ili kutii kiu zao bila mafanikio. Katika kuhangaika huko, Adili alifika pahala akakutana na jumba kubwa lililozungukwa na ukuta mpana wa takribani futi arobaini, huku juu ukifikia futi ishirini. Ukuta huo uliuzunguka mji wa mawe. Baada ya kuingia humo ndani, alikumbana na habari nzito ambazo, Shaaban Robert amezisimulia kinaganaga. Walakini, bila kutwawilisha muda,


## PITIO LA VITABU



**Na: Maundu Mwingizi (Mwanabalagha), Mtu wa Tabora.**

itoshe tu kusema kwamba baada ya jitihadi zake

zilizoletwa na ujasiri, hatimaye



**SHABAN ROBERT 1901-1962**

akiwa amejipatia mali nyingi mno pamoja na msichana mrembo kupita kiasi. Shaaban Robert anatujulisha kwamba, kama uzuri wote wa peponi wamejaaliwa Malaika, basi karibu uzuri wote wa duniani alijaaliwa msichana huyo.

*Itaendelea toleo lijalo*

# Tangazo

**PATA NAKALA ZA VITABU VYA RIWAYA KATIKA SEHEMU ZIFUATAZO**

**DAR ES SALAAM:**

- Duka la Kona ya Riwaya—Kinondoni

  **Tel: 0655 428 085** –Zamira

- Posta Mpya Karibu na mzunguko wa Askari

  **Tel: 0755 454 152** George

**MOROGORO:**

- Kituo cha Daladala, Bima Samaki Samaki

  **Tel: 0748 623 743**

**ARUSHA:**

- Wakala nje ya duka la Kimahama
  Tel: 0757 690 302

**MBEYA:**

- Duka la vitabu FANANI na HADHIRA
  Tel: 046 840 840

**IRINGA:**

- Fika Stationary kubwa ya LUTENGANO


Soma kitabu kikukomboe kifikra na kimtazamo


**Simu: +255766974865**
**Insta: jamvi la Simulizi**
**Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

**Ngurumo ya Mwandishi**
**S.L.P 1039**
**Iringa**
**Whatsapp: +255734550514**


**Msanifu wa Jalada: Nnepei Graphics — 0624310506**

## MTUNZI WETU: LATIFA NTANGA



Ninaitwa Latifa Ntanga, mtoto wa kwanza kwenye familia ya watoto wanne. Nimezaliwa Dar es salaam, lakini ni mwenyeji wa Songea. Kwa elimu, mimi nimeishia darasa la saba. Nimesoma shule ya msingi Liwiti iliyopo tabata. Kwa sasa ninaishi Chanika.

Kwa kweli sikuwahi kutaraji kuwa mwandishi. Ilitokea kwa sadfa tu nikaanza kuandika kama masihara. Lakini kadri nilivyokuwa naandika ndipo akili ikawa inafunguka zaidi, nikawa napata *idea* mbalimbali na hapo nikaendelea kuandika. Nimeanza kuandika mwaka 2015.

Katika uandishi nakutana na changamoto nyingi sana ikiwamo usumbufu kutoka kwa wanaume, kutukanwa pale ninapouza simulizi na pia kukosa sapoti kwa waandishi wenzangu.

Mimi ninaandika sana riwaya za dhati zinazojikita kwenye maisha, mapenzi na ujasusi kidogo. Lakini pia huwa naandika zaidi Simulizi zinazohusiana na maswala ya ndoa. Huko ndiko nilikoikita kalamu yangu.

Mpaka sasa nimechapa vitabu viwili; Machungu Yasiyosahaulika na Kichaa cha Ndoa. Lakini nina Simulizi nyingine kama Ndoa ya Maumivu, Mke Mwenza, Ndugu wa Mume, Mgumba, Mwanaume wa Usiku, Mrembo Mcharuko na Sifai Kuwa Mke.

Wapo wanawake wengi wenye vipaji vya kuandika lakini wanatawaliwa na dhana ya uoga na ile isemayo mwanamke ni dhaifu. Hata Mimi nilipoanza kuandika nilikuwa naogopa na kufikiria je jamii itanielewa kweli maana imejengeka kwamba kila kitu ni wanaume, ndiyo wanaweza kufanya na asilimia kubwa waandishi wengi ni wanaume lakini na sisi lazima tuoneshe umahiri wetu. Jambo ninalowaambia wanawake wanaoona wana uwezo na kipawa cha kuandika na kutunga ni kuwa; waji-amini na watumie vipaji vyao kuelimisha jamii.

**Kwa ambaye atahitaji kitabu au simulizi za kawaida anaweza kunipigia**

**Latifa—0719618409.**